# CHUO CHA SANAA DAR ES SALAAM

*"Kipaji ni Ajira. Sanaa ni Biashara"*

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KOZI ZA AfterExams – SanaaTime, 2025

# KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

### 1. KUHUSU CHUO CHA SANAA DAR ES SALAAM

**Chuo cha Sanaa Dar es Salaam** ni Chuo cha kisasa kinachoongoza nchini Tanzania kwa kutoa mafunzo ya Sanaa za aina nyingi za Kitamaduni na za Kisasa, yanayojikita zaidi kwenye mazoezi ya vitendo yanayohakikisha kila mwanachuo bila ya kujali tofauti zake za umri, hali, nafasi, kipato, elimu na uelewa, anakuwa mahiri.

Kusoma **Chuo cha Sanaa Dar es Salaam** ni zaidi ya kujifunza; kwani Chuo kinaibua, kukuza na kuendeleza vipaji kuwa ujuzi wa kitaalamu. Pia huwasaidia wahitimu kujiajiri au kuajiriwa kupitia vipaji vyao. Chuo kinawaunganisha *(connection)* wanachuo na wasanii maarufu na taasisi zinazojishughulisha na Sanaa.

Hapa Chuoni ndoto ya kila mwanachuo katika Sanaa inaheshimiwa na kuwekewa mikakati mahususi ya kuhakikisha mbali ya kufundishwa, anasaidiwa kutimiza ndoto yake.

Chuo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (**NACTVET**) kwa namba **REG/NACTVET/1125**. Na kimeidhinishwa na Baraza la Sanaa la Taifa (**BASATA**) na Bodi ya Filamu Tanzania (**TFB**).

### 2. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo mkono wa kulia kama unatoka Kituo cha Mabasi cha Magufuli *(Mbezi)* kuelekea Kibaha, kando ya barabara ya Morogoro eneo la Kibamba, Dar es Salaam, Tanzania.

### 3. KOZI ZITOLEWAZO

**Chuo cha Sanaa Dar es Salaam** kinatoa kozi mbalimbali za Sanaa za muda mrefu na muda mfupi. Pia tunatoa kozi za Mahitaji Mahususi *(Tailor-made Courses)*, Usimamizi wa Sanaa *(Art management).* Tuna kozi za muda mrefu na muda mfupi. Tuna zamu za asubuhi, zamu za jioni, na madarasa ya nyumbani/ofisini. Kozi zilizoandikwa kwenye fomu hii ni baadhi tu ya kozi tunazotoa. Iwapo una maswali kuhusu kozi zetu, sifa za kujiunga, muda wa kujiunga, gharama za masomo, ofa na fursa tulizonazo, na mengineyo tafadhali usisite kuja Chuoni au kutupigia simu.

### 4. KUHUSU AfterExams – SanaaTime PROGRAMME

**After-Exams Sanaa Time** ni programu maalum ya **Chuo cha Sanaa Dar es Salaam** inayotoa mafunzo ya Sanaa kwa kwa vitendo kwa wanafunzi wa **Darasa la Nne, Darasa la Saba, Kidato cha Pili,** na **Kidato cha Nne** mara baada ya mitihani ya Taifa, wakiwa wanangoja matokeo. Programu hufadhiliwa na kampuni ya **Popular Vision Ltd** kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii (CSR), hivyo hutolewa kwa **punguzo kubwa la ada**.

Mafunzo yanalenga kuibua, kukuza, na kuendeleza vipaji kuwa ujuzi wa kitaalamu ili kuongeza nafasi na thamani yao katika soko la ajira kwa baadaye. Kozi imeandaliwa kitaalamu ili isiharibu mwenendo wa masomo yao ya shule, bali iongeze morali na ari ya kujifunza. Mafunzo ni ya vitendo, yanayojumuisha *mentorship* kutoka kwa wasanii wakongwe, ziara za mafunzo, na utayarishaji wa kazi halisi za Sanaa. Mafunzo haya ni **rasmi**, hutolewa kwenye mazingira **salama** na yenye **maadili** kwa watoto, na kila mhitimu hutunukiwa **cheti kinachotambulika**.

### 5. MUDA WA MAFUNZO

Kwa mwaka 2025 muda wa mafunzo utakuwa kama ifuatavyo:

- **Darasa la Nne:** Kuanzia tarehe 31/10/2025 hadi 27/12/2025.
- **Darasa la Saba:** Kuanzia tarehe 19/09/2025 hadi 20/12/2025.
- **Kidato cha Pili:** Kuanzia tarehe 21/11/2025 hadi 20/12/2025.
- **Kidato cha Nne:** Kuanzia tarehe 29/11/2025 hadi 28/02/2026.

Ratiba ya masomo ni kila siku za kazi kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni, na Jumamosi saa 2:00 asubuhi hadi saa 6:30 mchana. Hatufanyi kazi siku za Jumapili na siku za mapumziko ya kitaifa.

## 6. KOZI ZINAZOTOLEWA KWENYE PROGRAMU YA AfterExams – SanaaTime

Kwenye programu hii ya ofa, kozi zinazotolewa ni sita (6) tu, ambazo ni:

- Uigizaji wa Filamu;
- Kuimba Muziki;
- Upigaji wa Ala za Muziki;
- Uchoraji wa Picha na Mapambo *(Drawing and Decoration);*
- Ususi, Makeup na Mapambo *(Ornamentation);* na
- Ubunifu wa Mitindo na Uanamitindo.

## 7. VIFAA VYA KUANDIKIA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na *note book* yenye jalada gumu au *counter book* dogo *la size* ya A5, moja tu, lenye idadi yoyote ya kurasa na kalamu ya wino moja.

## 8. UTARATIBU WA UVAAJI NGUO CHUONI

Wanafunzi wanavaa Chuoni viatu na nguo za chini za nyumbani. Juu, wanavaa fulana rasmi za Chuo. Hata hivyo, **nguo zinazoonesha sehemu yoyote ya mwili kutoka kifuani hadi magotini pamoja na kwapa au zinazoonesha nguo za ndani** na **kandambili haziruhusiwi kuvaliwa Chuoni**. Wazazi wote wanaombwa kuhakikisha watoto wao wanavaa mavazi ya staha na yenye maadili wakati wote wanapokuja Chuoni.

## 9. VIPODOZI NA UREMBO

Utaratibu wa matumizi ya vipodozi na urembo ikiwemo kunyoa na kusuka nywele, yanafuata taratibu za Shule ambazo wanafunzi husika wanasoma. Wazazi wanaombwa kuhakikisha wakati wote watoto wao wanapokuja Chuoni wanakuwa nadhifu na wanafuata maadili, misingi na taratibu za Shule na familia zao.

## 10. MATUMIZI YA SIMU ZA MKONONI CHUONI

Wanafunzi hawazuiwi kuja na simu Chuoni. Chuo kinahimiza matumizi ya simu kwa maadili, uwajibikaji na heshima wakati wote. Lakini kama mzazi ana katazo kwa mtoto wake kuhusu kuwa na simu, anashauriwa kuendeleza katazo hilo na anaombwa kutoa taarifa Chuoni ili Chuo kisaidie kumsimamia mtoto wake.

## 11. ZANA/VIFAA VYA SANAA KWA MATUMIZI BINAFSI

Wanachuo wanaruhusiwa kuja Chuoni na zana au vifaa binafsi vya Sanaa wanavyopenda na wanavyomudu kumiliki kulingana na kozi wanazokuja kusoma, kwa ajili ya matumizi yao binafsi na wanarudi navyo nyumbani; lakini si lazima. Chuo kina zana na vifaa vya mazoezi ya vitendo kwa ajili ya wanachuo wake wote.

## 12. KUFANYA MAZOEZI YA VITENDO (*PRACTICAL*)

Sehemu kubwa ya mafunzo haya hutolewa kwa vitendo. Wanachuo huhudhuria sehemu mbalimbali kwa ajili ya kujizoeza kwa vitendo; hii ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye mashindano, sherehe, na maonesho mbalimbali.

## 13. GHARAMA ZA ADA NA VIFAA

| S/N | Ada/Kifaa | Gharama (TZS) |
|---|---|---|
| 1. | Ada | 60,000 kwa mwezi |
| 2. | Fulana ya Chuo | 20,000 |

## 14. MASUALA YA KUZINGATIA KATIKA MALIPO

a. Malipo yote yanapaswa kufanywa kwa kutumia **Namba ya Kumbukumbu** *(**Control Number**).*
b. Ada inaweza kulipwa kwa mkupuo mmoja au kwa awamu mara moja kwa kila mwezi wa masomo.
c. Chuo hakipokei malipo kwa fedha taslimu. **Katika mazingira yoyote, usikabidhi pesa taslimu au kwa simu kwa mfanyakazi yeyote wa Chuo kwa ajili ya kulipia chochote.**
d. **Malipo yoyote yakifanywa, hayawezi kuhamishwa wala kurejeshwa**.

## 15. NYARAKA ZA KUWASILISHA KWENYE USAJILI

Anapokuja kuripoti, Mwanafunzi anatakiwa aje na picha mbili *(passport size)*, nakala kivuli ya Cheti cha kuzaliwa, nakala kivuli za vyeti vyovyote vya kitaaluma alivyonavyo mwanafunzi husika.

## 16. ZINGATIA

Chuo kinaongozwa na Sheria Ndogo, Kanuni, Taratibu na Maadili ambayo wanachuo wanapaswa kuyatii.

## 17. KWA MAWASILIANO ZAIDI

Kwa maelezo zaidi tutembelee Chuoni au kwenye tovuti yetu www.dararts.ac.tz au tupigie simu **0715 910 010.**